Jiwe la kirohola kujenge Na 40

## MUNGU ANA TAFUTA APATE TABIA

***Mwanzo 24:1*** *"Basi Abraham alikuwa mzee, mwenywe. Miaka mingi na bwana alikuwa amembariki Abrahamu katika vitu vyote"*

Yesu ana hesabu tabia,sio wingi wa watu, unajuwa hilo? Yeye anahesabu tabia.Mungu siku zote anajaribu kupata mtu mmoja mkononi mwake.Hicho ndicho kitu anachohitaji. Anachohitaji ni mtu mmoja naye ataifanya kazi yake katika miaka yote hebu fikiria Yeye alipata mtu mmoja mwenye haki katika siku za Nuhu, Katika siku za Musa alipata mtu mmoja mwenye haki.
***(2 Nyakati 16:9)***Mungu anatafuta tabia, sio watu wengi, ni tabia. Eliezar alipokuwa anaenda kumtafutia Isaka bibi harusi ***(Mwanzo24:1-9)*** alilitokea jasho hilo mpaka akapata tabia, Kumbuka Abraham alimpa wajibu kama vile Mungu anavyotupa wajibu sisi wahudumu tuliomtafutia bibi harusi Mungu aubariki moyo wake mimi siangalii wingi wake wa watu
nangalia walio safi katika moyo. Mtu fulani ambaye atakiamini neno
***(Mathayo 5:8).*** Eliezar aliangalia naye akawaza hili siwezi kulifanya mimi mwenyewe natambuwa kuna majukumu makubwa. Nina tambuwa wajibu wakumtafutia Isaka… Ambao ni mfano wa kanisa. Unajuwa? Kristo, Rebecca ni mfano wa bibi harusi na Eliezar akapiga magoti kuomba na akasema "Mungu inabidi unisaidie mimi" na alipokuwa anamuangalia Mungu, Mungu alimsaidia akapata tabia.

Rudi kwenye neno ndugu mrudunieni Mungu, usikilize hilo kanisa ambalo wewe ni mwana chama wake. Unaweza ukaka pale kama atakuruhusu, lakini jambo la kwanza ni kuja kwa Mungu, hiyo ni sahihi. Eliezar alipopata ile tabia ambayo ilikuwa ndani ya yule mwanamke Rebecca, bibi harusi wakupendeza wa Isaka alimwambia habari za Isaka na hakuhoji hata kitu kimoja. Aliamini lile neno la mjumbe na akajiweka tayari kwenda (***Ufunuo 19:6-8)*** na wakaenda wakamuomba baba yake naye akawaambia muulizeni huyo mwanamke mwenywe. Muulizeni yeye, uamuzi wake na uwe ndio huo (***Mwanzo24:57-59)*** Mwanamke akasema nitakwenda". anakwenda wapi kwa mwanaume ambaye hajamuona kamwe wala hajajuwa chochote juu yake ***(Petro 1:8-9)*** lakini bado yule mwanamke alikuwa tayari, kwa sababu alichaguliwa Kimbele, hiyo ni sawa kabisa unaweza ukanisikia mimi nikihubiri huu ujumbe, unaweza kumuona Roho Mtakatifu akipambanua siri za moyo na akifanya mambo akifanya mambo makuu na akitenda miujiza. Unaweza ukaomba na bado isiende kutendeka, endelea mbele thawabu yako

inakuja mwishoni. Si itakuwa ni jambo zuri wakati huo? Ndiyo , Tazama , mfanyie Yesu huduma, huo ni ujumbe wakati wa mwisho , yeye anaye bibi harusi, Mungu anatafuta tabia na Eliezar alipopata tabia kitu kilichofuatia alimfanya kuwa tayari kwenda kwenda hilo ni sawa. Na sasa ndugu, jambo lile lile lina ujumbe wa wakati wa mwisho.Utapitia Bibliani. Mungu siku zote anatafuta tabia sio wanadamu,Leo tunafanya kinyume chake tunatafuta wingi wa wanachama waliovaa vizuri badala ya kufuata tabia. Eliezar alilitolea jasho hilo mpaka alipopata tabia. Hiyo ni kweli alipata mtu wa namna gan? Naye alimtegemea Mungu. Tabia kwa ajili ya nini, tabia kwa Isaka, kwa bibi harusi, ambalo kanisa ni mfano unajua hilo, Hiyo ilikua mzao wa kimwili wa Ibrahimu; Huu ni uzao wa kifalme wa Ibrahimu ***(Galatia 3:7-29)*** vema kama Eliezar yule mjumbe wa wakati wa mwisho akijaribu kumtafuta , bibi Harusi wa Kristo hata angalia wanachama wa kidhehebu. Ataangalia tabia ya watu walio tayari.

Angalia tabia iliyo nzuri kwanza, Halafu amfanye yule mwanamke kukutana na Isaka, baada ya kuwa amempata anamfanya yule mwanamke asimame kwa utulivu kwa muda mrefu wakutosha kusikiliza ujumbe wake, ambao ni wa Isaka ***(Isaya 30:15;Zaburi 23:2)*** Huyo ni mjumbe wa siku za mwisho ile nuru ya wakati wa jioni, na kwanza tafuta hilo kanisa (mahali ambapo wataamini ule ujumbe) liwinde hilo, liwinde upate kujua hilo kanisa liko wapi, ambalo litakuruhusu uje ndani, ambalo halitafunga milango usoni pako na halafu unapofanya hapo sasa umepata tabia, sasa kama utasimama kwa utulivu muda wa kutosha kumueleza vile bibi harusi anayopaswa kuvalishwa! Inabidi kumueleza vile bibi Harusi anavyopaswa kuvalishwa! Inabidi avalishwe nguo, Asimame kwa utulivu, Muangalie Rebecca mdogo alivyosikiliza kila neno, moyo wake mdogo ulikuwa unadundadunda, Alikua akimuelekeza yeye (Eliezar alikua akimuelekeza Rebecca) Sasa umelitokea jasho. "Nitaenda wapi" Mpaka nitakapoona tabia. Halafu ninapoiona tabia, sasa mfanye asimame kwa utulivu muda mrefu wa kutosha kumfanya awe tayari kwenda kukutana naye. Oh! Jamani, oh ni kitu cha ajabu namna gani! Mfanye awe tayari, Asimame kwa utulivu kuskiliza ujumbe wake kumhusu Yeye, Eliezar hakua anajizungumzia mwenyewe, Bali alikua anamzungumzia mmoja aliyemtuma. Sasa alikua na vipawa kuthibitisha kwamba ametumwa kutoka kwake. Amen! Alitaka kumvalisha yule mwanamke na hivi vitu, unajua vile ambavyo alimtengeneza Yeye. Muangalie yule mjumbe wa siku za mwisho kazi yake itakuwa ni kuwafanya watakatifu wawe tayari, yule Bibi harusi awe tayari kwa Bwana harusi huo utakuwa ujumbe wake. [1]

Kuzungumza juu ya washirika leo watu wanachotaka ni washirika. Mungu haangalii washirika, Mungu anatafuta tabia, kwamba angeliweza kuliweka neno

lake kwa mtu fulani ambaye atamuamini yeye. Kama nilivyosema usiku ule mwingine.Eliezar alilitolea jasho mpaka akapata tabia kwa bibi harusi, Halafu ilibidi amfanye yule mwanamke atulie ili aweze kumvalisha kwa namna iliyo sahihi kukutana na yule mmoja ambaye alikua anazungumzia habari zake. [2]

Nilisema Eliezar alitolea jasho hilo mpaka akapata tabia ndani ya Rebeka. Halafu sasa ilimpasa amvalishe yule mwanamke awe tayari, alipaswa amfanye atulie na kusikiliza ujumbe wake. Tatizo lililopo leo, unapopata tabia ni vigumu kuwafanya wao watulie muda wakutosha kuweza kuwavalisha nguo na wawe wamevalishwa, hiyo ni kweli, anakuja Ricky mdogo tayari ameanza kuwavuta wao anawaondoa anawapeleka upande mwingine hiyo ni kweli lakini pale Eliezar alilitolea jasho. [3]

Biblia ilisema mkewe amejiweka tayari ***(Ufunuo 19:7)*** Pale mwisho wa wakati alijiwekaje mwenywe tayari ilikuwa mkewe? Na anatakiwa afanye nini? Ni aina gani ya vazi ambalo amevaa? Neno lake mwenywe , Alikua amevalishwa katika haki yake ***(Ufunuo 19:8)*** Hiyo ni sahihi, unaona? [4]

Sasa angalia hapa natumaini ataivisha taji huduma yangu taji na hili la kuniacha nichukue nguo za neno na kumvalisha bibi harusi katika nguo za neno na kwa haki yake ***(Wakolosai 3:10-15)*** Natumaini atanivalisha taji na kunifanya na kuniacha nisimame pale katika siku ile na kusema "Tazama mwanakondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu" ***(Yohana 1:29)*** [5]

Mwanadamu anaangalia vizuri muonekano , unachanganya na hiyo ndio maana mwanamke alipewa huo uzuri, kwaajili ya udanganyifu ili adanganye. Mwanamke mzuri kama hautumii huo uzuri wake kwa namna iliyo sahihi , ni laana kwake, ambayo itampeleka motoni haraka sana kuliko kitu kingine chohote nikijuacho, kama anaweza akawa mzuri sawa, ilimradi anakaa na mume wake na kufanya kilicho sahihi hilo ni zuri na la kupendeza, lakini anaweza akalichukuwa jambo hilohilo na jamii! Na jinsi anavyoweza kudanganya kwa hilo kwasababu alipewa hilo kufanyia hivyo. Angalia, sasa Mungu anajieleleza kwa tabia "Yeye hana umbo wala uzuri hata tumtamani Yesu" ***(Isaya 53:2-3***) lakini kamwe hakujawa na tabia kama ya kwake hapa duniani. Sasa tunaona leo tabia ya kanisa Shetani na kundi lake, wanaangalia kile ambacho ni kikubwa! Makanisa mazuri makubwa, makubwa, vitu vizuri hivyo ndivyo dunia inayoangalia Leo. "oh! yule Mchungaji mtu mkubwa ,fulani na wakati fulani na fulani amevaa kikuhani hasa na kiungu anatembea na Joho lake kubwa na mambo kama hayo" Wanaita huo uzuri, lakini watakatifu halisi wa Mungu wanaangalia tabia ya neno lililothibitishwa [6].

Na kuwaona wao, nimekuja na hitimisho hili haijalishi ukoje, haijalishi kile ulicho, inabidi Mungu awape waskilizaji. Haijalishi kama ningesimama asubuhi hii ya leo na kuwatafuta watu waliokufa na kuwafanya viwete watembee katika hali yao ya kawaida na kama Mungu hayuuko kwenye huo mpango hautaweza kuendelea ipasavyo Mungu awe kwenye huo mpango hautaweza kuendelea. Inapaswa Mungu awe kwenye huo mpango, tabia yake inajulikana kwa kazi zake, haijalishi yeye ni nani kazi zake zinathibitisha tabia yake kama utamchukuwa mtu haijalishi anajaribu kujifanya mzuri kama kazi zake ni uovu. Uzuri wake hautafika popote.Na maneno ya mtu ndiyo tabia yake. Mtu ambaye neno lake siyo zuri hapa sasa hatakuwa na imani na huyo mtu kwasababu maneno yake sio mazuri. Kwahiyo sasa Mungu baba yetu tabia yake na kazi zake zinathibitisha kile alicho (7).

Kama mimi ni Mkristo, ninabidi nitambulishwe na kila tabia ya biblia, inanipasa nisimame na Nuhu na kuhubiri pamoja naye katika siku zake nikiwaonya watu, hiyo ni kweli inabidi nisimame katika mlima Kalmeli peke yangu pamoja na Eliya. Inabidi nisimame msalabani na nisulubishwe katika utu wangu na mawazo yangu pamoja naye ***(Warumi 6:6)*** Lakini sasa tena nimefufuka pamoja naye katika siku ya pasaka nikiwa mshindi juu ya vitu vyote. [8]

Mungu atuhurumie sisi kama ni wana na binti za Mungu, Nasi tuwageni katika hayo maisha……… Mungu anangalia tabia kwa wanaume na wanawake ambao wanaweza kuishi wenyewe kama wana binti wa mfalme. Mungu atuhurumie sisi, kwamba tutafanya hivyo, hilo ndilo ninalolitafuta mara si tabia, Hicho ndicho Mungu anachotuvutia tabia, kwajili ya bibi Harusi ambaye atanyakuliwa. Na sisi kama wana na binti za Mungu tuenende kama hilo kuwa na binti! Mungu atusaidie sisi. [9]

**NUKUU KINGEREZA**

1. Uinjili wa siku za mwisho (62-0603) aya 193,197-201,213,243-249
2. Utambulisho (63-0123) aya ya 199-200
3. Mara moja tena bwana (63-0120E) aya 125
4. Uchungu wa kuzaa (65-0124) aya 196
5. Kiwango cha sasa cha huduma yangu (62-0908) aya ya 1216
6. Ndoa na talaka (65-0221M) Aya 141-144
7. Amini kutoka moyoni (57-06230 Aya E-9
8. Wakati wa mavuno (64-12120 Aya 202
9. Ushuhuda baharini (62-0720) Aya E-28

Jiwe la kiroho la kujengea na. 40 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, Yamekusanywa na Gerd Rodewald friedenstr. 69 D-75328 Schomberg, Germany Simu (+49) 72357613 Fax: (+49) 72353306

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyokusudiwa kimbele imesikia.

(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)

*Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:*

*Charles E. Y. Kanju.*

*Box 553 Korogwe - Tanga*

*E-mail: Chaelika@livel.com*

*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*